



TANZANIA HIGHER LEARNING INSTITUTIONS TRADE UNION  
P.O. BOX 35928 DAR ES SALAAM, Tanzania  
Tel: 022 2401581, Fax: 022 2401582  
Website [www.thtu.or.tz](http://www.thtu.or.tz), Email: [info@thtu.or.tz](mailto:info@thtu.or.tz)

## **TAHARUKI YA KIKOKOTOO CHA MAFAO YA KUSTAAFU: TATIZO LIMESHALEWEKA, SASA TWENDE KWENYE SULUHISHO**

### **Utangulizi**

Hivi karibuni, umeibuka mjadala mkali juu ya mafao ya watumishi wanaostaifu ajira baada ya mfuko mpya wa PSSSF kuanza kufanya kazi. Mjadala huo unajikita kwenye kikokotoo cha mafao ambacho kinapunguza mafao yanayolipwa kwa mtumishi aliystaifu. Mjadala huu ambao umetawaliwa na hisia kali umepelekea kurushiana lawama kwa taasisi na wadau wote wanaohusika na sekta ya hifadhi ya jamii. Ni wazi kabisa kwamba Vyama vya wafanyakazi vimelaumiwa, Bunge limelaumiwa, Serikali imelaumiwa na Mamlaka ya hifadhi ya jamii (SSRA) imelaumiwa. THTU tunaamini kwamba kuacha hili jambo liishe bila muafaka ni kutojitendea haki sisi kama Taifa lenye watu wakomavu na waliostaarabika. Kimsingi, mjadala wa mafao ya kustaifu limekuwa likijirudia mara kwa mara bila muafaka wa pande zote na hivyo kuendelea kuacha hisia za kurushiana lawama.

THTU tunaamini kwamba jambo hili liko ndani ya uwezo wetu kama Taifa kulipatia muafaka na ufumbuzi wa kudumu. Kwa msingi huo, tunapenda kuungana na wafanyakazi wote nchini na umma wa Tanzania kutoa maoni yetu machache kama kichocheo cha kuhamisha mjadala kutoka kulaumiana kwenda kwenye suluhisho ili hatimae hali ya utulivu irejee.

1. Awali ya yote, tunakiri kwamba tulishiriki kikamilifu kutoa maoni yetu wakati wa kuandikwa sheria iliyouna mfuko wa PSSSF. Tunaishukuru na kuipongeza Serikali pamoja na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Kamati ya Huduma za Jamii kwa kutumia zaidi ya masaa matatu kusikiliza maoni yetu (wakati huo). Maoni mengi tuliyotoa kama chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu yalizingatiwa kwenye sheria husika. Tunathubutu kusema kwamba tunaikubali sheria iliyounanisha mifuko. Ni bahati mbaya sana kwamba uundaji wa kanuni ambazo ndizo zenye vikokotoo haukuwa shirikishi kwa upande wetu sisi THTU. Hata hivyo, tunaamini bado muda upo wa sisi kutoa maoni yetu kwa lengo la kuboresha

2. Mjadala mkubwa ulioibuka baada ya mfuko wa PSSSF kuanza kazi umejikita katika vikokotoo vinavyoshusha mafao ya mkupuo kwa wastaafu hasa kwenye kipengele cha asilimia sihirini na tano (25%).
3. Ileweke kwamba ni kweli Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) imejitahidi sana kuboresha mafao hasa kwa Mifuko ya PPF na NSSF ambayo ndiyo ilikuwa inalipa mafao kidogo sana kuliko mifuko mingine kabla ya kuunganishwa
4. Mfano mzuri ni kikokotoo cha PPF ambacho awali kilikuwa **1/960**; baada ya majadiliano na SSRA na mfuko husika ikawa **1/600** na mwaka 2014 SSRA ilisawazisha kikokotoo kwa mifuko yote ikawa **1/580 isipokuwa kwa watumishi wa mifuko ya LAPF na PSPF kabla ya Julai 2014 ambao walibaki na 1/540**. Ndio maana wakati huo Profesa aliyefanya kazi kwa zaidi ya miaka 30 akichangia mfuko wa PPF alilipwa fao la mkupuo la milioni isiyozidi ishirini na tano (25,000,000) wakati mtumishi aliystaafu akiwa PSPF/LAPF alipokea milioni sitini mpaka mia moja. Mfano huu pekee utupe faraja kwamba majadiliano ya pamoja huleta suluhisho lenye manufaa kwa pande zote
5. Baada ya vikokotoo kusawazishwa mwaka 2014, wale watumishi waliokuwa wakichangia mifuko ya PSPF na LAPF kabla ya Julai 2014 waliruhusiwa kubaki na kikokotoo chao kilichokuwepo ambacho ni **1/540**, miaka 15.5 na 50% ya fao la mkupuo. Kikokotoo kilichosawazishwa ni 1/580, miaka 12.5 na 25% ya fao la mkupuo. Hii ina maana ilitengenezwa makundi mawili katika ulipaji wa mafao ya kustaafu.
6. Baada ya mfuko wa PSSSF kuanzishwa, kikokotoo kilichosawazishwa na ambacho kilianza kutumika mwaka 2014 kimeondoa yale makundi mawili yaliyokuwepo hasa kwenye vipengele vya asilimia na miaka. Hii ina maana kwamba wastaafu wote wanaanza kutumia kikokotoo cha **1/580**, miaka 12.5; 25% ya fao la mkupuo na 75% ya pensheni ya kila mwezi. Kwa msingi huu, walioathiriwa zaidi na kikokotoo kipyga ni wale walikuwepo kwenye mifuko ya PSPF na LAPF kabla ya Julai 2014. Kundi hili lililoathiriwa limesaidia kutoa picha halisi ya mafao ya hifadhi ya jamii baada ya mtumishi kustaafu
7. Sisi THTU tunaamini ukweli huu uliodhihirika au ulojidhihiru wenyewe unapaswa kuangaliwa kwa jicho la pekee na kurekebishwa kwa mjadala wa pamoja. Wizara husika kupitia SSRA inaweza kuratibu zoezi la kupokea maoni ya wadau wote kwa lengo la kurekebisha kikokotoo kilicholeta tararuki na hivyo kutuliza wafanyakazi. SSRA imeshafanya mikutano mingi na wadau hasa wafanyakazi kupitia vyama vyao tangu

ilipoanzishwa. Majadiliano ya pamoja itapelekea uwepo wa muafaka wa pamoja na kuacha kulaumiana.

8. Sisi THTU tunatoa pendekozo la kuanzia kuelekea mjadala wa pamoja kwamba kikokotoo KIBORESHWE ili kuondoa makundi yaliyopo sasa. Pendekozo letu la kuboresha kikokotoo ni **1/540**, miaka **15.5** na **50%** ya fao la mkupuo na **50%** inayobaki iwe pensheni ya kila mwezi. Bahati nzuri SSRA imetoa ufanuzi mzuri kabisa kwamba kwa kikokotoo cha sasahivi, mstaafu atalipwa pesa zake zote kwa utaratibu wa 25% mkupuo na 75% kila mwezi. Kumbe mwisho wa siku mstaafu atalipwa pesa zake zote. Mjadala wa pamoja ujikite kwenye swali hili; **Je! Tunaweza kuboresha kikokotoo kikawa 50% ya mkupuo na 50% iliyobaki ikaingia kwenye pensheni ya kila mwezi?** Maeneo mengine yanayolalamikiwa yatajadiliwa kwenye mjadala wa pamoja.

### **Hitimisho**

Ni pendekozo letu THTU kwamba sasa tatizo limeshafahamika. Tuhamishe mjadala kutoka kulaumiana kwenda kwenye suluhisho. Sasa tuunganishe nguvu na akili zetu kutafuta suluhisho. Mwalimu Nyerere anatuasa kwamba **tujisahihishe**. Tusiogope kujisahihisha. Sisi tumeanza na pendekozo. Tunawaalika wadau wote kuelekea kwenye mjadala wa pamoja kupata muafaka wa pamoja. Hakuna linaloshindikana, tutimize wajibu wetu.

### **Muhimu:**

*THTU itakutanisha wataalamu wa sekta ya hifadhi ya jamii ili kuandaa mapendekozo ya kina na kuwasilisha SSRA na Wizara husika kwa ajili ya mjadala na ufumbuzi. Tunaamini mapendekozo yetu yanaendana na malengo ya kulinda afya za muda mrefu ya mifuko na pia kutimiza malengo ya hifadhi ya jamii.*

---



DKT Paul Loisulie  
MKT THTU Taifa